




# USAID

KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI



## TANZANIA **HESABU NA ELIMU JUMUIISHI**

Pamoja na maendeleo katika kukuza usawa na upatikanaji wa elimu nchini Tanzania, stadi za msingi katika kusoma na kuhesabu zinabaki kuwa na changamoto ya kila siku kwa wanafunzi wengi. Mradi wa *Hesabu na Elimu Jumuishi* umeundwa kuboresha mafunzo ya hesabu kwa watoto katika madarasa ya chini na kushughulikia mahitaji ya elimu jumuishi kwa watoto wenye ulemavu. Mradi huu unatokana na mradi wa USAID wa Tusome Pamoja kusaidia elimu jumuishi katika maeneo ya mradi na kutoa msaada wa kitaalamu, vifaa vya kufundishia, na msaada kwa wanafunzi shulenii na darasani.

Walengwa wanaonufaika ni pamoja na wanafunzi wote wa darasa la 1 na 2 pamoja na waalimu na viongozi wa elimu katika shule za msingi za serikali. Wakipatiwa mafunzo endelevu, wanafunzi watapatiwa ujuzi wa hesabu katika mpangilio jumuishi.

*Hesabu na elimu Jumuishi* inafanya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar, Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa – Idara Maalum (Zanzibar), na sekretarieti za mikoa.



# USAID

KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI

## MALENGO YA MRADI

Malengo ya Hesabu na Elimu Jumuishi yamebuniwa sambamba na vipaumbele vya Mkakati wa Kitaifa wa Serikali ya Tanzania ya Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya elimu Jumuishi. Malengo hayo ni pamoja na:

- Kutoa vifaa sahihi na muhimu vya kufundishia na kujifunzia hesabu;
- Kufanya kazi na waalimu katika kutumia zaidi vifaa vya hesabu kwa ufanisi kufundishia na kujifunzia darasani;
- Kufanya kazi na shule kutoa uongozi, usimamizi, mafunzo, na ushauri katika kusaidia ufundishaji wa hesabu;
- Kutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na mbinu za mafunzo ambazo huzingatia mahitaji ya watoto wenye ulemavu; na
- Kuhakikisha kuwa watoto wenye ulemavu hawakumbani na unyanyapaa au ubaguzi katika shule zao na jamii na wanapata na kushiriki katika masomo.

## MATOKEO YANAYOTARAJIWA

Mwisho wa mradi, tunatarajia yafuatayo:

- Kufikia zaidi ya walimu 10,000 na vifaa vya kufundishia na kujifunzia, na mafunzo kuititia mitaala ya hesabu iliyokubaliwa kitaifa kuhusu namna ya kutoa msaada mzuri wa kielimu kwa watoto wenye ulemavu. Vifaa hivi vinajumuisha kitengo kimoja cha nyongeza kwa kila darasa na nakala moja ya mtaala wa hesabu kwa waalimu kwa kila darasa;
- Zaidi ya wanafunzi 700,000 watanufaika na vifaa vya kufundishia na mbinu za mafunzo za hesabu.

**BAJETI** Dola za Marekani milioni 13.5

### MUDA

Oktoba 2019 – Januari 2021

### MAENEKO YA MRADI

- Morogoro
- Iringa
- Mtwara
- Ruvuma
- Zanzibar

### WABIA WA UTEKELEZAJI

RTI International

<https://rti.org/>

### MSHIRIKA

Serikali ya Tanzania

### MAWASILIANO YA USAID

Abbas Nsanzugwanko  
Afisa Mkataba Mwakilishi  
+255 22 229 4006  
[ansanzugwanko@usaid.gov](mailto:ansanzugwanko@usaid.gov)

### MAWASILIANO YA MBIA

Stephen Backman  
Mkuu wa Mradi  
RTI International  
+255 756 786 426  
[sbackman@rti.org](mailto:sbackman@rti.org)

### KWA MAWASILIANO ZAIDI

Tovuti: [www.usaid.gov/tanzania](http://www.usaid.gov/tanzania)  
Facebook: USAIDTanzania  
Twitter: @USAIDTanzania